


# ZABURI KWETU

## Wakati wa Kwarezma

Mwaka B

Toni Iragi K


Février 2024

# Zab 24-Mapito yako ee Bwana

1er DTC-B

Muziki : Toni Iragi K







1. Ee Bwana, unionyeshe njia za**ko,**
unijulishe na mapito ya**ko.**
Uniongoze katika uaminifu wako, unifundi**she,**
maana Wewe ndiwe Mungu mwokozi wa**ngu.**

2. Ee Bwana, ukumbuke huruma ya**ko,**
na rehema zako, maana ni za kale na ka**le.**
Unikumbuke kwa kadiri ya huruma ya**ko,**
ee Bwana, kwa ajili ya wema wa**ko.**

3. Bwana ni mwema, tena mwenye ha**ki,**
kwa hiyo awajulisha waovu nji**a;**
awaongoza watu maskini katika ha**ki,**
awafundisha wanyonge njia ya**ke.**

# Neno lako ee Bwana

## Shangilio la Enjili/Acclamation 1er DTC-B


Muziki : Toni Iragi K



# Zb 105-Nitatembea mbele ya Bwana

Siku ya Mungu ya pili ya Kwaresma

Muziki : Toni Iragi K




1. Naliamini hata nilipose**ma:**
Mimi nimesumbuka **mno".**
Kina bei kubwa machoni pa Bwa**na**
kifo cha waamini wa**ke.**


2. Ee Bwana, mimi mtumishi wa**ko,**
umenifungulia vifu**ngo.**
Nitakutolea sadaka ya si**fa,**
nitaliomba jina la Bwa**na.**

3. Nitamtimizia Bwana naziri za**ngu**
mbele ya taifa lake lo**te,**
katika wanja za nyumba ya Bwa**na,**
katika boma lako, ewe Yerusale**mu.**

# Sifa kwa Kristu

## Acclamation de l'Evangile-2è & 3è DTC-B

Toni Iragi K



# Zb 18b-Ee Bwana wewe unayo maneno

## Siku ya Mungu ya tatu ya Kwarezma B

Toni Iragi K




1. Sheria ya Bwana ni kami**lifu,**
   yatuliza **roho;**
   mafundisho ya Bwana ni i**mara,**
   yamletea mjinga e**limu.**

2. Amri za Bwana ni za **haki,**
   zafurahisha **moyo;**
   agizo la Bwana ni **safi,**
   layatia macho mwa**ngaza.**

3. Ibada kwa Bwana ni **safi,**
   yadumu hata mi**lele;**
   hukumu za Bwana ni **kweli,**
   zote za haki ka**mili.**

4. Zatamanika kuliko za**habu,**
   kuliko wingi wa zahabu **safi;**
   ni tamu kuliko **asali,**
   kuliko mavuno ya **uki.**

# Zb-136 Yerusalemu ndani ya roho yangu

4è DTC-B

Muziki : Toni Iragi K




*1.* Kando ya mito ya Babeli, ndiko tuli**kokaa**
na kulia machozi, tulipokumbuka **Siyoni**
Katika miti iliyo**kuwako**
tulitundika vinu**bi vyetu.**


2.Maana huko waliotu**hamisha**
waliotuomba nyimbo waliotusumbua, **furaha :**
« Haya, tuimbeni wimbo wa **Siyoni ».**
Tuimbeje wimbo wa Bwana katika nchi ya **Kigeni ?**

3. Nikusahau, ee Yeru**salemu,**
mkono wangu wa kuume na usaha**uliwe.**
Ulimi wangu uambate kaaka**ni mwangu,**
nisipokukumbuka wewe, nisipoweka Yeru**salemu**
juu ya furaha ya**ngu yote.**

# Sifa na utukufu

## Acclamation de l'Evangile/4è, 5è DTC-B & Rameaux/Matawi

Toni Iragi K



# Zb-50 Utupatie roho mpya

5è DTC-B

Musique : Toni Iragi K




1. Unihurumie, ee Mungu, kwa wema wa**ko ;**
kwa wema yako kubwa, ufute maovu ya**ngu**.
Unioshe kabisa kosa la**ngu,**
unisafishe pia zambi ya**ngu.**


2. Uniumbie moyo safi, ee Mu**ngu,**
utengeneze tena ndani yangu roho ima**ra.**
Usinitupe mbali na uso wa**ko,**
wala usiniondoshee roho yako takati**fu.**

3. Unirudishie furaha ya wokovu wa**ko,**
unisabitishie roho kari**mu.**
Nitawafundisha waasi njia za**ko,**
nao wakosefu watakuongoke**a.**

# Zb-21 Kwanini umeniacha?

Siku ya Mungu ya Matawi

Toni Iragi K




1. Wote wanaoniona wa**nicheka,**
wanacheka, na kutiki**sa kichwa:**
" Alimwamini Bwana, naye a**mwokoe,**
amwopoe, kwani a**nampenda!**

2. Kwa maana mbwa wengi wameni**zunguka,**
kundi la waovu wana**nisonga:**
wamenitoboa mikono na **miguu,**
naweza kuhesabu mifupa ya**ngu yote;**

3. Wanagawanya nguo zangu ka**ti yao,**
wanaipigia kura ka**nzu yangu.**
Nawe, ee Bwana, usisima**me mbali!**
Ewe Bwana msaada wangu, fanya haraka kunisa**idia!**

4. Nitawahubiri ndugu zangu ji**na lako,**
katikati ya mkutano nita**kusifu!**
Enyi watumishi wa Bwana, **msifuni.**
Enyi watumishi wa Bwana, **msifuni.**

# Mwana kondoo wa Mungu

## Agnus Dei

Archidiocèse de Bukavu
Paroisse de Kavumu

Muziki : Toni Iragi K

